



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

MAPITIO YA SITA YA KISEKTA YA UKIMWI MWAKA 2014

Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, na Wadau wa Maendeleo imeandaa Mkutano wa sita wa kutathimini utekelezaji wa sekta ya udhibiti wa UKIMWI nchini. Mkutano huu utajadili mafanikio, Changamoto na utekelezaji wa Mkakati wa tatu wa kudhibiti UKIMWI (NMSF III 2013/18). Mkutano wa Kisera utakaofanyika Tarehe 17-18/11/2014 utatunguliwa na Mkutano wa Kitaalam utakaofanyika tarehe 11-13/11/2014 katika Ukumbi wa Mikutano Wa Ubungo Blue Pearl.

Mkutano huu utawashirikisha wawakilishi kutoka Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, Mashirika ya Umma, Wadau wa Maendeleo, Mitandao ya Watu wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI (WAVIU), Asasi zisizo za Kiserikali, Asasi za Kijamii na Kidini, Sekretariat za Mikoa na Serikali za Mitaa, Jamii na Taasisi za Tafiti na Elimu ya Juu.

Mkutano huu hufanyika kila baada ya miaka miwili kujadili maendeleo ya kisekta ya utekelezaji wa mipango ya kudhibiti UKIMWI, changamoto na kuainisha utekelezaji wa vipaumbele vya baadae kulingana na Mkakati wa tatu (NMSF III 2013/18) wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI, MKUKUTA na Malengo ya Maendeleo ya Millenia na Sera nyingine zilizopo. Kauli mbiu ya Mwaka huu ni **"Mwitikio Endelevu wa Udhibiti wa UKIMWI Kufikia Sifuri Tatu"**.

Mkutano huu utajadili kwa upana katika maeneo ya kimkakati yafuatayo; Kinga, Matunzo, Matibabu na Msaada, Mazingira wezeshi, Kupunguza Athari za UKIMWI, Ufuatiliaji na Tathmini na Utafutaji na Rasilimali Watu na Fedha.

Mkutano wa pamoja wa mapitio ya sekta ya UKIMWI utajadili mwelekeo na Mwenendo wa ugonjwa wa UKIMWI kwa Mwaka 2013/14, taarifa ya mapato na matumizi katika mwitikio wa UKIMWI wa taifa, ugharamiaji wa huduma za UKIMWI na taarifa ya mwitikio wa Taifa.

Mkutano huu utaongozwa kwa pamoja kati ya Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu na Kiongozi wa Kundi la Wadau wa Maendeleo ya UKIMWI. Inatarajiwa kwamba mwisho wa mkutano huu tutakubaliana malengo na vipaumbele vya utekelezaji kwa miaka miwili ifuatayo (2015-16).

IMETOLEWA NA
MWENYEKITI MTENDAJI
TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA
(TACAIDS)